JUA
GAZETI LA MAENDELEO
Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 21 - Toleo la 448

Kuhusu majadiliano ya chumba cha raïa huko Kinshasa

Twajua sote ya kama yapata miaka mitatu, nchi ya Zaïre yakabiliwa na mizozo na shida za kila aina. Maisha yaendelea kuwa magumu siku baada ya siku sababu ya wanasiasa wasiopenda nchi na wanaotaka kutawala na kuishi vile watakavyo kwa kutaka kutafuta jawabu, wana-Zaïre ao wanasiasa wa Zaïre wapima tangu wakati mwingi kutatua mzozo lakini hawafaulu kwa nia zao mbaya.

Tukichunguza majadiliano, inayofanyika kwa sasa mjini Kinshasa na kuona namna yanavyoendeshwa, twaofu kwa mara ingine na kusema *kama* bahati mdogo sana ili wanasiasa waelewane. Ingawaje tume ine kwa jumla ya sita zilikwisha toa ripoti zao na pande zote mbili kukubaliana kwa mambo ambayo yaleta uwasiwasi na yasiyoeleweka inayoweza taifa la Zaïre tena baada ya kupatana katika giza kuu. Hatujui ikiwa waliacha kwa makusudi ao kwa kusahahu kufaamisha kwanza ukomo ao chanzo cha mzozo ulioko nchini ; kwa kutokuheshimu sheria inayoongoza, iliyotokana na "CNS" pia na majadiliano ya pamoja ya wanasiasa (compromis politique global). Hali hiyo ndiyo iliyotuma nchi ikawa na bunge mbili, serkali mbili, waziri wakuu wawili na kazalika. Tena katika mkataba huo wa sheria, wajumbe wa pande zote hawakufaamisha ni mapaswa gani rais wa jamuhuri ataendesha wakati huu wa mpito, nani atakayeongoza jeshi la inchi pamoja na diplomasia.

Katika madaraka ya rais wa jamuhuri, tume hizo ziliwayi tu kusema kazi ya rais pasipo kueleza yale atakayofanya. Tena wajumbe wote kakubaliana kama maoni ya kura (référendum populaire) itafanyika mbele ya kiserkali (projet de constitution) ambayo watu hawajui kama itakuwa ya "CNS" ao ile ya "Conclave". Na ikiwa ratiba mpya iktakuwa, itaandikwa na nani na kufuatana na hali gani? Hayo yote ni maswali yanayobidi kupata jibu.

Ingawaje mengi yamekwisha kuongoka, inayobaki ni kujua nani atakayekuwa waziri mkuu, wakati kila tume lazingatia mjumbe wake yaani Tshisekedi na Birindwa. Kwa ngambo ya upinzani, inafaa Tshisekedi kuwa waziri mkuu kwa vile kachaguliwa na "CNS" ambayo kachagua pia Monsengwo na kumupa madaraka kwa miaka miwili rais Mobutu.

Kwa nini wasemavyo moja aweza kukataa mwengine? Huo ndio ukweli wa wapinzani. Kwa ngambo ya upande wa rais (mouvance) haifai Tshisekedi kuwekwa tena nafasi ya waziri mkuu sababu hakuweza kutii sheria, na ndio sababu baraza la "Conclave" kamteuwa bwana Birindwa kwa vile aanzishe mabadiliko ya pesa ambayo twasikia kama zaïre 1 ni samani ya zaïre milioni 3, na dolari 1 samani ya zaïre 3. Hata hivyo pesa hizo haziwezi kutoa Zaïre katika shida ikiwa hakuna mazao na benki zakosa pesa.

Mutungwa Abandelwa Phóly

Wamama wachuuzi ni wevi !

Ni mda wa miaka 10 sasa wamama wachuuzi wa nguo (Cotebu, Dubay, Sotexki, Superwax...) na hasa pia wamama wa Zaire kwenda Burundi na Ishasha wanaiba sana kwa nia yao mbaya ya kuwina haraka, kupata faida ya pesa bila kukawia, ao kutoa jasho !

Vitu viwili vinavyoangaisha wamama hao wevi ni kwanza tamaa ya mwili (kuburudika) na pupa kali ya pesa, vinavyowatuma kuwazarau waume wao nyumbani hata kwa mwisho tumeona mmoja kati yao kufikilia kumu uwa mme wake. Kwa nia gani ? Kwa nia tu yakubaki huru na kutangatanga kama mabata ndani ya maji, magari; barabarani na vilaboni wakinywa pombe na kupanda popote mbegu mbaya ya ukahaba na kusafirisha kiini cha ukimwi.

Wengi kati ya wamama hao hawamuogopi Mungu aliyewaumba kwa sababu wategemea nguvu za shetani na mitishamba. Wengi twawaona kushuka hata kuzimuni wakitafuta nguvu za shetani kwa kuwina mbiombio, kujiuzia nyumba na kuwapevusha bwana wasio wao kiisha kumuondoa maishani mmewe wa nyumbani, bwana wa ndoa!

Lakini tabia hiyo siyo kwa wote. Umalaya na kushirikiana na mizimu ni tabia za wengi kati yao. Lakini ni vema tushuhudia kama wengi zaidi ni wevi . Angalia wale wamama wachuuzi wa viatu barabarani. Wakubali haraka kutenda uzinifu kwa tamaa ya pesa. Anasa za dunia ! Mifano na majina yao ni mengi. Angalieni pia wamama wachuuzi wa mafuta ya "Chief, Canola..." tokea njia ya Rwanda. Hao wafynza mafuta hayo na shindano ama iliyopungukiwa na litri moja ao zaidi. Wamama wachuuzi wa mafuta ya kujipakaa (glycÇrine, parfum...) na pia mafuta ya taa. Nao pia watumia nusu na kutia maji ndani ya chupa isiyojaa.

Enendeni kunako soko na maduka ya "bwaki" mtaani Kadutu mkajioneee namna gani vibweta na chupa vyauzishwa kwa matumizi hiyo mbaya ya wizi. Pia, nguo (kitenge) yakatwa na kuuzishwa "changachanga". Wamama wachuuzi, jiheshimuni hii ni shauri pia kwa wachuuzi wa madawa sokoni na dukani ! Siku za mwizi na msharati ni harubahini !

Imata Raphaël Déwen

Afya: dawa kwa ugonjwa wa malaria

Ni jani moja toka huko Uchina liitwalo "quinghoa" ambalo laaminika na sasa kuwa dawa halisi kwa ugonjwa wa maleria. Shirika la afya ulimwenguni (OMS) lilijulisha kama dawa hiyo itahusika na kuokoa tangu mwaka wa 1994, maisha ya watu yapata 100.000 kwa mwaka ulimwenguni nzima. Silaha mpya hiyo, ilikwisha kujaribiwa barani Afrika na Asia ambako kaonyesha ubingwa wake. Ugonjwa huo ndio wahatarisha maisha ya watu wengi katika nchi za joto : yapata watu milioni 270 wanao na wengine yapata milioni 1 wafariki kila mwaka kutokana na maleria. Uwingi wa vijidudu vikali katika miili na visivyokubali matibabu, hasa barani Afrika vyaleta uwasiwasi.

Shirika hilo la afya ulimwenguni kajulisha pia ya kwamba magonjwa ya ukoma yapunguka . Ikiwa mwaka wa 1960 idadi ya wagonjwa wa ukoma ilikuwa ya watu milioni 10, mnamo mwaka wa 1991. Wagonjwa kaonekana yapata milioni 5 na nusu tu. Nchi ya Nigeria barahi Afrika na ya Brezilia bara Amerika ndizo zilizo na idadi kubwa ya wagonjwa. Barani Asia (huko mashariki ya kusini) nchi ya India yaonekana kuwa yasumbuliwa zaidi na ugonjwa ule. Shirika la afya kajulisha ya kuwa yapata watu 3.446 wanao ukoma nchini Uturuki(Turquie) na mtu 1 nchini Uswisi.

Yanayoshambulia wengi zaidi barani Afrika ni magonjwa ya moyo(crises cardiaques) ambayo yatawala hivi polepole kufuatana na maelezo ya tume moja la kiganga la mjini Ufaransa. Tutafahamisha kuwa ni nchi ya Pwani ya Pembe ao "Côte d'Ivoire" inayoendesha vipimo halisi ya mishipa hiyo ya moyo.

Toka MFI

Na Mutungwa Abandelwa Phóly

UHARIRI

Tujenge taifa letu

Maazimio ya mkutano mkuu wa majadiliano na masikilizano muhimu kunako jumba la raia mjini mkuu Kinshasa yakawia. Anayelipenda taifa lake apaswa kulitumikia na kulijenga kwa bidii na moyo wa huruma kwa manufaa ya raia waishimo daima.

Maana matetezi, maandamano na maneno ni bure pasipo matendo, kazi bora, zamiri ya kazi na roho ya ujenzi. Je ! Ni nani waziri mkuu nchini kwa kesho ? Hizuru nani, mwana-Zaïre anayelipenda na kulitumikia taifa lake. Yule asiyependelea tu wanasiasa wa kabila lake ao wa jimbo lake kwa sababu Zaïre inayo majimbo 11. Tujenge taifa letu na kutupilia mbali ubaguzi wa makabila, rangi yá ngozi, fujo na migombano.

Katika jimbo kuu la Kivu ya Kusini, wanasiasa waliotumia uongo, hasira na nguvu ya kuwashambulia wenzao na matusi wapo wapi leo ? Twawaona barabarni wakitangatanga, wakijuta, wasijui watakuwa wageni wa nani. Sababu raia wamevumbua kama siasa yao ya chuki na mazarau ilikua haramu ! Waheshimiwa hao wa jana wasema eti mtu ni mtu, usimzarau mwenzio ao kumpiga na kumshambulia ingawa amechagua cháma fulani kidemokrasia isiyolingana na maitaji yao. Shal kumbe wadikteta ni wengi na wajivika ngozi ya kondoo ?

Tujenge taifa, tutumike vizuri tukitupilia mbali matusi na tamaa ya mali ya jirani. Chama kinachomunga mkono baba wa taifa letu kama vile chama cha upinzani, vyote vyapigania madaraka, hukumu, kuishi katika anasa, uongozi wa watu, na kazalika. Ni vema viongozi wasikilizane kwa kusaidia raia katika kazi ya utafuti wa masikilizano na ujenzi wa taifa.

Nchini mwetu Zaïre tulioachiwa na mababu hakuna jamaa mbili ya wanasiasa. Wote wanasiasa hao wamemtumikia miaka karibuni 30 na prezidenti mmoja ambae kawafunza namna ya kujitetea, namna ya kuimarisha uhusiano kati ya Zaïre na nchi za kigeni, pia namna yakulinda raia katika ukinya, kuwanyonya pesa na mali yao, kuiba mali ya serkali na kutupilia mbali magumu yetu.

Tusidanganywe kila siku. Wanasiasa wajipendelea na hakuna anayependa raia nchini Zaïre. Wote watia mbele jamaa zao, mifuko yao, wandugu wao kikabila...basi tuombe Mungu awaangazie waache tabia hiyo na wajenge taifa !

Imata Raphaël Déwen

Je, umesikia ... ?

KUWA, yapata zehebu na madini za kikristo 15 vyapigania kustawi huko Lugushwa ambako kwapatikana zahabu nyingi mtaani kote Mwenga na ambako wachimba magodi watwaa vifaa vyao kuenda mitoni? Yasemekana mnamo mwezi wa septemba kuwa ni wafuasi wa "papa Simon, Aidini na waamini wa Mungu aliye hai" kakataliwa sehemu hiyo inayokaliwa na watu wasiofikilia 500. Viongozi wa sehemu hiyo kawaambia hao eti dini katoliki na zehebu zingine mbili tu za kiprotestanti zatosha kwa kuihubiri habari njema.

KAMA, ni baada ya mda mchache tu, viongozi wa serkali na wale wa michezo katangaza kwa pupa kutengenezwa kwa kiwanja cha kandanda cha Kadutu? Huko kikikataliwa kufunguliwa sababu ya kuilainisha na kupanda majani (pelouse) kama ilivyojulishwa na tume moja maarufu. Kwa sasa, kiwanja hicho ki utupu na maji ya kisonga polepole hapa warugaruga wa Nyamugo wachezea. Hata hivyo michezo ya kandanda yaendeshwa huko Nyakavogo. Ukweli uko wapi wakati watu wajiuliza wapi iliyoenda "carburant" iliyokusanywa kwa kufanya hima. Hakuna nguvu yoyote kwa upande ule. Wachezaji pamoja na kiwanja chao hawana lolote la kusema.

KWAMBA, yanayopitika kisiwani Idjwi yafaa kuchunguzwa kwa makiji sana viongozi wa serkali. Yaseme kana huko kama shirika moja la maendeleo lapingana na kiongozi wa mtaa huo na mwami wa asili wake. Na hiyo si mara ya kwanza? Kwa sasa, tume la haki na amani linalosaidiwa na kikundi la Bahavu (mutuelle Havu) kalalamika na kuwachafua Mwami Ntambuka na kiongozi wa mtaa huo ya kuwa wavunja haki za wanainchi kwa kuwapiga bakora na kuwafunga pasipo sababu zaidi kuwapokonya feza zao. Kwa ngambo yao, viongozi wahukumu mabingwa wa makundi hayo isiyojulikana na isiyotii sheria ili kwamba mtaa huo uendeshe kazi zake inavyostahili. Nani anayo sheria na nani astahili kuhukumiwa? Ni kweli, ndiyo sasa wakati wa kuamua.

ETI, kufuatana na kukimbia ya watu kazaa wanasheria, kama viwanda ao shirika na watu wengi wajifanyawevi halisi mjini Kindu-Molunge? Huko wakijipa sheria eti hawapokei, watu haona mashika hayo yaruhusu wakuu wao wa mjini Kinshasa kupokea mishahara ya mashirika ya serkali iliyoko maniema. Na hiyo wakiaidia wafanyakazi mjini kindu kulipwa mishahara yao. Ingawaje hivyo watumishi wa BCZ, Azap na wale wa Budget waliachozi la damu na maji kupata mishahara yao kwa bwana Narasha wa "Entriaco" na huko kunako "BAT-Zaïre". Inayobaki ni kujua kama hayo yatokana na ukosefu wa pesa ao wa zamiri safi.